

3 : TAUHEED AL-ASMAAI WASWIFAAT (MAJINA YAKE ALLAH NA SIFA ZAKE).

Maana yake ni kuamini majina yote ambayo Allah (sw) amejiiita yeye mwenyewe na kujisifu kwayo, au aliyoitwa na kusifiwa na Mtume wake Muhammad صلى الله عليه وسلم , na kuthibitisha hivyo katika hali ambayo inalingana na utukufu wake Allah (sw) bila ya kupindisha, wala kukataa ambacho ni wajibu kwake Allah, wala kumfananisha Allah na sifa ya viumbe, katika hali ya uhakika sio majazi, na kukanusha yale ambayo Allah (sw) yeye mwenyewe amekanusha na kukataa, au zile sifa ambazo Mtume wa Allah amezikanusha na kuzikataa, na zile ambazo hazijathibitishwa wala kukataliwa ni wajibu mtu kujiepusha nazo, haifai kuthibitisha wala kukanusha.

MIONGONI MWA MIFANO YA MAJINA YAKE ALLAH (SW).

Allah (sw) anayo majina mazuri aliyojiita yeye mwenyewe kama vile Allah yu hai na niwa tangu, kwa hiyo ni wajibu kwetu kuamini kuwa Allah yu hai, kwamba uhai ni miongoni wa sifa zake Allah (sw), nayo ni uhai ulikamilika ambao haujatanguliwa na kukosekana uhai wala kuisha kuwa uhai wake umekoma.

Mwenyezi mungu amejiiita kuwa ni mwenye kusikia (Assami'u), hapa ni wajibu juu yetu kuamini kuwa Allah (sw) kusikia ni sifa yake na ni jina miongoni mwa majina yake subhanahu wata'ala na kuwa Allah anasikia.